

Karibu kwa Maktaba ya Hadhira

Maktaba ya hadhira ni mahali ambapo kila mtu anakaribishwa. Kwenye maktaba, wewe na jamii yako mnaweza kupata habari, kusoma au kujifunza, kuuliza maswali mbalimbali, kuhudhuria vipindi mbalimbali, kukopa vitabu...na mengineyo!

Ukiwa kwenye maktaba, wewe pamoja na jamii yako mnaweza...



Kukopa vifaa vya habari vikiwemo:

- Rasilimali zakujifunza Kiingerereza
- Kanda za DVD, muziki na vitabu vya kusikiza
- Vitabu, magazeti... na mengineyo!



Kutumia kompyuta

Maktaba mengi yana kompyuta ya baruapepe na mtandao ya intaneti. Maktaba zingine zina kompyuta ya kuandika wasifu na mabarua, kujifunza lugha na mengineyo.



Kutumia rasili mali za mtandao ya intaneti

Maktaba zingine zina rasilimali za mtandao maalum pamoja na hifadhidata. Unaweza kusikiza na kusoma vitabu kupitia kwa kompyuta, kusoma magazeti na majarida.



Kupata vitabu na magazeti katika lugha mengi

Maktaba zingine zina vitabu, magazeti, na rasilimali zingine kwa lugha mengi. Uliza kwenye maktaba yako kwa habari zaidi



Kuhudhuria vipindi vya maktaba

Maktaba nyingi zina vipindi, madarasa na mradi mbalimbali za watoto, watu wazima na jamii nzima. Leta watoto wako kwenye maktaba ili wadumuishwe na hadithi. Maktaba nyingi pia zina vilabu vya kusoma vitabu, madarasa ya kujifunza kompyuta kwa watu wazima, na mradi mengine pia. Uliza kwenye maktaba yako kuhusu mradi walizo nazo.



Pata majibu kwa maswali yako

Wafanyi kazi wa maktaba wanaweza kukusaidia kupata majibu ya maswali kadha wa kadha. Tafadhali, uliza tu.



Tafuta Maktaba ya Hadhira karibu nawe.

Kuna maktaba ya hadhira zaidi ya 100 katika mkoa wa Manitoba.

Maktaba ya Hadhira ya Winnipeg

Maktaba ya Millennium (Tawi Kuu)
251 Donald Street, Winnipeg

Simu: 204-986-6450

Mtandao ya intaneti: winnipeg.ca/library

Tuna malokesheni kwa sehemu zaidi ya ishirini(20). Maktaba ya Millennium ndio kubwa zaidi ikiwa na vifaa zaidi ya 650,000, pamoja na vitabu katika lugha zaidi ya thelathini(30)

Maktaba ya Jimbo la Magharibi la Manitoba

Tawi ya Brandon (Tawi Kuu)
710 Rosser Avenue Unit 1, Brandon

Simu: 204-727-6648

Mtandao ya intaneti: wmrl.ca

Tuna malokesheni ndani ya Carberry, Neepawa, Glenboro na Hartney.

Maktaba ya Jimbo la Kusini ya Kati

Tawi ya Winkler (Tawi Kuu)
160 Main Street, Winkler

Simu: 204-325-7174

Mtandao ya intaneti: scribriary.mb.ca

Tuna malokesheni ndani ya Altona, Morden na Miami.

Maktaba ya Jake Epp

255 Elmdale Street, Steinbach

Simu: 204-326-6841

Mtandao ya intaneti: jakeeplibriary.com

Kupata maktaba zingine katika mkoa wa Manitoba, piga simu (bila malipo)

1-800-252-9998

Mtandao ya intaneti: gov.mb.ca/chc/pls/index.html

Je, nawezaje kupata kadi ya maktaba?

Kadi ya maktaba inaonyesha kwamba wewe ni mwanachama ya maktaba. Enda kwa maktaba yako na ulete kitambulisho ili upate kadi ya maktaba. Kadi ya maktaba hupewa bure bila malipo. Tafadhali uliza kwenye maktaba yako kuhusu habari ya kuwa mwanachama.

- Kitambulisho inaweza kuwa leseni ya udereva, kadi ya Afya ya Manitoba, au kitu inacho onyesha mahali unapoishi.
- Weka kadi yako mahali pema na uripoti kadi zilizopotea kwenye maktaba.

Je, nawezaje kukopa vifaa vya maktaba?

- Vifaa nyingi ndani ya maktaba yanaweza kukopwa. Ukikopa kifaa kutoka kwa maktaba utapewa muda na tarehe ya kuirudisha. Tarehe ya kurudisha inapofika, ni lazima kifaa kirudishwe kwenye maktaba.
- Tafadhali rudisha vifaa vya maktaba kwa hali nzuri kwa ajili watu wengine watazitemia.

Je, itakuaje ikiwa nimechelewa?

- Ni muhimu sana kurudisha vifaa vya maktaba kwa wakati. Unaweza kulipa faini ikiwa umechelewa kurudisha vifaa.
- Wakati nyingine, unaweza kutumia vifaa vya maktaba kwa muda mrefu zaidi. Uliza kwenye maktaba yako jinsi ya kupanua muda ya vifaa ulizokopa.

Shirika la Maktaba yako: